



Nani Ambao Wangepokea “Teacher of Distinction Award 2015” Wilaya ya Meru?

In this issue:

4

Life Skills Corner: Mtaala wa Haiba na michezo na matumizi ya sanduku la zana(toolkit); Mafunzo ya Kubalehe

8

Habari Kutoka Mashuleni: Darasa Saidizi la K.K.K.; Learning Support Unit Project

10


TFFT Ikisherekea Siku ya Mtoto ya Umoja wa Mataifa: Makao 12 ya watoto yalipongezwa

Utafutaji wa mwalimu bora mwaka 2015 huambana na tuzo ambaye hutolewa kila mwaka na shirika la The Foundation for Tomorrow kwa walimu wa shule za serikali na binafsi katika ngazi ya elimu ya msingi and sekondari.

Lengo la tuzo hii ni kutia hamasa na changamoto kwa walimu katika mchakato mzima wa kufundisha na kujifunza kwa wanafunzi wetu mashuleni. Kadhalika kutambua jitihada za walimu katika utekelezaji wa majukumu yao kila siku kama inavyo wapasa kufanya.

Zoezi hili la utafutaji wa mwalimu bora mwaka 2015 katika wilaya ya Meru lilianza mwezi Agosti kwa kuhusisha hatua mbali mbali kama vile uandaaji wa vigezo vya kuzingatia, ujazaji wa fomu ambaye ulikuwa huru kwa mwanafunzi, mwalimu au uongozi wa shule na wazazi pia walipata fursa ya kupendekeza mwalimu anaye stahili na kukizi vigezo katika tuzo hii. Hii ni kuhakikisha pia wazazi wanahusika katika maendeleo ya kitaaluma kwa watoto wao.

Lengo la tuzo hii ni kutia hamasa na changamoto kwa walimu katika mchakato mzima wa kufundisha na kujifunza kwa wanafunzi wetu mashuleni.



“A good teacher can inspire hope, ignite the imagination, and instill a love of learning.”

Utafutaji wa mwalimu bora mwaka 2015 huambana na tuzo ambaye hutolewa kila mwaka na shirika la The Foundation for Tomorrow kwa walimu wa shule za serikali na binafsi katika ngazi ya elimu ya msingi and sekondari.

Lengo la tuzo hii ni kutia hamasa na changamoto kwa walimu katika mchakato mzima wa kufundisha na kujifunza kwa wanafunzi wetu mashuleni. Kadhalika kutambua jitihada za walimu katika utekelezaji wa majukumu yao kila siku kama inavyo wapasa kufanya.


Zoezi hili la utafutaji wa mwalimu bora mwaka 2015 katika wilaya ya Meru lilianza mwezi Agosti kwa kuhusisha hatua mbali mbali kama vile uandaaji wa vigezo vya kuzingatia, ujazaji wa fomu ambaye ulikuwa huru kwa mwanafunzi, mwalimu au uongozi wa shule na wazazi pia walipata fursa ya kupendekeza mwalimu anaye stahili na kukizi vigezo katika tuzo hii. Hii ni kuhakikisha pia wazazi wanahusika katika maendeleo ya kitaaluma kwa watoto wao.

Pia zoezi hili lilihusisha maafisa elimu kata (Ward Education Officers- WEOs) ambaye walihusika kusambaza fomu katika shule

zote za msingi na sekondari zilizopo kwenye kata zao ilikutoa fursa ya kupendekezwa kwa walimu kupitia kujaza fomu hizo. Kulikuwa na zaidi ya walimu 200 waliopendekezwa kwa shule zote za wilaya ya Meru na kuorodhezwa kufikia walimu 32 waliokidhi vigezo. Hatua iliyofuata ni kuwafanyia mahojiano (interview), kupitia muktasari mbalimbali kama vile azimio la somo, andalio la somo, zana za kufundishia na ufundishaji (micro teaching) kwa kila mwalimu ilikujua zaidi ufundishaji wake darasani na hatimaye kufikia walimu 10 ambaye watapokea tuzo hii ya Mwalimu Bora Mwaka 2015.

Kwa sababu mbalimbali kama vile uchaguzi mkuu Oktoba 2015 na walimu kuhusika na michakato ya kusimamia na kusahisha mitihani ya taifa imechangia na kusababisha kucheleshwa kwa utoaji wa tuzo hii kwa wakati uliopangwa. Hivyo kwa mujibu wa sababu hizi tumeshindwa kutoa na kukabidhi tuzo kwa walimu husika kama ilivyo kusudiwa hapo awali. Lakini bado washindi wote wa tuzo hii ya mwalimu bora watakabidhiwa tuzo zao mapema Januari 2016.

Some pictures from the “Teacher of Distinction Award” deliberation procedure
 One thing we have seen through this award proceedings is that there is no shortage of creative teachers in Meru District!





Life Skills Corner

By: Hilda B. Lema
TFFT Full Circle Program
Manager

Mtaala wa Haiba na michezo na matumizi ya sanduku la zana(toolkit)

Jarida letu lililochapishwa June lilieleza kwa undani kuwa tumeandaa mtaala wa haiba na michezo utakaotumika katika vipindi vya haiba na michezo kwa kila darasa. Hii ilijumuisha mafunzo ya siku nne yaliyotolewa na TFFT kwa waalimu 2 kila shule kati ya zile zilizopo kwenye mradi wa majaribio. Pia kila shule ilipatiwa sanduku moja(toolkit) lenye vifaa vya kufundishia na vifaa vya michezo.

Hivi karibuni nimepata nafasi ya kuingiza shule ya Sinai katika mradi huu wa majaribio. Shule hii ni moja ya shule iliyopo chini ya uangalizi wa TFFT. Shule hii ilipatiwa mafunzo, haya mafunzo yalinifurahisha kwa sababu kila mwalimu ata wale wasiofundisha somo la haiba walihudhuria. Mwisho wa mafunzo waliona umuhimu wa kutilia mkazo ufundishwaji wa somo la Haiba. Japo wana mwalimu mmoja tu anayefundisha Haiba madarasa yote wamekubaliana watashirikiana wote kufundisha ili somo.

Shule hizi 10 za majaribio zilipatiwa mtaala wa haiba kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba kwa shule za serikali uliandaliwa katika lugha ya kiswahili na shule binafsi mtaala huu uliandaliwa kwa lugha ya kiingereza. Hii imerahisishia waalimu wanaofundisha hili somo kwa sababu serikali imetoa mtaala mmoja tu uliojumuishia madarasa yote, hivyo inabidi kupokezana. Mtaala huu ulioandaliwa na TFFT madhumuni yake siyo kuchukua nafasi ya ule wa serikali au kupinga bali ni msaada kwa mwalimu kurahisishia ufundishaji. Mtaala huu umeshiba shughuli/mazoezi mbalimbali yanayopaswa kufanywa katika mada tofauti na jinsi ya kuzifanya na vifaa vinavyohitajika ambavyo vinapatikana ndani ya toolkit(sanduku).

Kwa kutumia huu mtaala mpya waalimu wanaofundisha Haiba

(continued)

***“Stadi za maisha
zitawasaidia
wanafunzi kufanya
maamuzi sahihi,
kuendeleza tabia
nzuri, kutatua
matatizo, kuwa na
ujasiri na kujiamini.”***

na michezo wanafurahia kwani huu mtaala umerahisishwa kwa namna ambayo inawezesha wepesi wa kufundisha Haiba.

Muda ambao nimekua nikifuatilia na kuchunguza utekelezaji na matumizi ya huu mtaala na toolkit katika hizi shule 10 za majaribio, nimegundua na kuona mafanikio yaliyo wazi (yanayoonekana kwa macho). Waalimu wamebadilisha mfumo wa kufundishia somo la haiba na masomo mengine. Wanatumia somo kwa vitendo, na ufundishaji shirikishi. Katika baadhi ya shule za serikali waalimu wanaarifu kuwa wanafunzi wale watoro wameanza kuhudhuria shule kutokana na michezo na vifaa vya michezo vilivyotolewa na TFFT. Kipindi cha nyuma waalimu hawakupenda kufundisha Haiba na kufundisha somo kwa vitendo kwa sababu vifaa vilivyohitajika havikuwepo, kwa sasa toolkit tuliyowapatia ina vifaa vyote vinavyohitajika kufundisha Haiba na Michezo. Wanafunzi wanafurahia kwa sasa wanasoma somo la Haiba vizuri ukilinganisha na kipindi cha nyuma ambacho vipindi vya Haiba vilikua vinatumika kwa shughuli nyingine.

Waalimu hawachukulii tena hili somo la Haiba kama mzigo kwa sababu wamekwisha andaliwa katika namna ya kufundisha, sasa kwa kuwa wameshaona umuhimu wa kufundisha wanafunzi Stadi za maisha (life skills) wanatamani kuona huu mtaala ukitumiwa na nchi nzima ili wanafunzi wote wajifunze stadi za maisha ambazo ni muhimu kwa maisha yao ya kila siku.

Mafunzo ya Kubalehe

Kipengele muhimu cha elimu ya



Mafunzo ya kubalehe na tabia hatarishi shule ya msingi Sylus Anderson, Sakila

stadi za maisha ni mwamko wa mabadiliko ya kubalehe. Miezi miwili iliyopita mimi na Noah tuliendesha mafunzo ya kubalehe na tabia hatarishi kwa wanafunzi wa darasa la 5&6 katika shule ya msingi Sylus Anderson moja ya shule zetu za majaribio. Nliamua kulingana na uzoefu wangu juu ya hii mada tuwatenganishe wanafunzi, wavulana wafundishwe na Noah na wasichana niwafundishe mimi lengo kuu ni kuwapa nafasi ya uhuru wa kujieleza na kuuliza maswali. Cha kushangaza wanafunzi wote walikataa na kudai wako huru kuchanganywa.

Japo tuliwachanganya Noah alifundisha sehemu zilizogusa wavulana na mimi sehemu zilizogusa wasichana. Yalikua ni mafunzo ya kipekee ambayo tuliwahi kufanya. Wanafunzi walikua na shauku ya kujifunza na waliuliza maswali mengi sana bila uoga au aibu.

Waliahidi kuwafundisha wadogo

zao na marafiki juu ya kubalehe na tabia hatarishi na jinsi ya kuziepuka. Yafuatayo ni baadhi ya maswali yaliyoulizwa na wanafunzi:

- Je inawezekana kukwepa hedhi?
- Ni kitu gani kitanipata nisipopata hedhi? Je nitakufa au kuwa mgumba?
- Je kujamiana ni muhimu mtu anapokua katika kubalehe?
- Wazazi wangu ni masikini na hawana uwezo wa kuninunulia pedi, ninatumia vitambaa vya kanga chakavu na hiki kipindi cha masika vitambaa havikauki, nifanyaje niweze kujisaidia, njia nyingine salama na nafuu isiyo na gharama nayoweza kutumia ni ipi?

Mafunzo ya Haki za Watoto

Waalimu hawajawezeshwa



Mafunzo ya Haki za Watoto, shule ya msingi Maji ya Chai

kikamilifu kufundisha baadhi ya mada zilizopo katika somo la haiba. Hakuna mafunzo yaliyotolewa wakati hili somo lilipoanzishwa mwaka 2005. Kwa kupitia mradi wa Full Circle ambao unashughulika na elimu ya stadi za maisha, baadhi ya shule ziliomba msaada wa kufundishwa kwa baadhi ya hizo mada ikiwemo Haki za Watoto. Mimi na Noah tulifundisha Haki na Wajibu wa mtoto katika shule ya Maji ya Chai, kwakweli yalikuwa ni mafunzo yenye mafanikio kwetu sote lakini zaidi kwa wanafunzi.

Mimi na Noah tulikaa na kupanga ni jinsi gani tunaweza tukafanikisha ufundishaji wa hii mada kwa malengo ya kuwezesha wanafunzi wa maji ya chai kuelewa haki na wajibu wao, na kupigania haki zao endapo zitakiukwa, pia kuelewa kama watoto pia wana majukumu ya kufanya. Nafikiri utakubaliana na mimi kuwa, “*kila palipo na haki lazima pawe na jukumu linaloendana na hiyo haki*”. Kama watoto wadogo wana jukumu la kujua haki zao na majukumu yao wakiwa nyumbani, shuleni na katika jamii

kwa ujumla.

Mafunzo haya yalichukua saa moja kwa kila darasa. Nilifurahia sana uchu wa hawa wanafunzi kutaka kujua haki zao kama watoto. Wakiwa katika makundi wanafunzi walipata nafasi ya kujadili na kubadishana mawazo juu ya wanachojua juu ya haki za watoto, kipi cha kufanya ikiwa haki zao zitakiukwa.

Ni katika njia mbali mbali, watoto wanakua na ufahamu juu ya haki zao na wajibu wao. Wanajifunza kuwa kama watoto wana haki ya kupata elimu na pia wanalo jukumu la kujifunza kama uwezo wao unavyoruhusu na pale inapobidi kushirikisha wengine uelewa wao.

Kwa kupitia haya mafunzo wamejifunza kuwa kama watachukua jukumu la kujifunza na kusoma watapata kiu itayopelekea kutimiza na kufikia ndoto zao. Pia walijifunza kuwa wao ndo viongozi wanaotegemewa na taifa ili leo na kesho. Wanatambua uongozi ni kuchukua na kutekeleza majukumu na siyo kutoa visingizio.

Kuanzishwa kwa kluba za stadi za maisha kwa shule za sekondari

Kwa upande mwingine wanafunzi wa Sekondari hawakuachwa nyuma kwenye stadi za maisha (life skills). Mwezi uliopita tulifanikiwa kuandaa mwongozo wa kufundishia masomo ya stadi za maisha na kuanzisha kluba 2 katika shule mbili za sekondari. Arusha Modern na Oldonyosambu. Katika hii programu ya Full Circle tuliona kuna umuhimu wa kuwa na kluba za stadi za maisha ambazo zitawezesha kuwepo na vipindi vitakavyo shughulikia mada muhimu ambazo hazifundishwi katika mazingira rafiki ya shule.

Mafundisho ya stadi za maisha katika shule za sekondari hayapewi kipaumbele. Wanafunzi wanalalamika hawafundishwi kulingana na maisha watakayoishi baada ya kumaliza shule. Wanapata maarifa ya darasani lakini kiuhalisia maarifa ya kukabiliana na maisha baada ya masomo yamefumbiwa

macho. Nafasi hii ya kipekee itawasaidia kujifunza baadhi ya stadi muhimu za maisha ikiwemo Ujasiriamali, Kuweka na kutekeleza malengo, kujiamini, Mawasiliano Fanisi, Kujiandaa kwa mitihani na Usimamizi wa Msongo.

Tulifanikiwa kuanzisha klabu za Stadi za maisha katika shule ya Arusha morden na Oldonyosambu. AMS tuna wanachama 28 kuanzia kidato cha kwanza adhi cha tano na Oldonyosambu tuna wanachama 45 kidato cha 1-3. Tayari wamechagua viongozi wa klabu na mwalimu msimamizi.

Uongozi wa hizi shule na waalimu wana hamu sana ya kuwa na hizi klabu. Wanasema ni nafasi ya kipekee na ya thamani kwa wanafunzi wao

Niliwapa baadhi ya maswali ili kupima ni kwa kiasi gani hizi klabu zinahitajika. Baadhi ya maswali yaliyoulizwa ni kama yafuatayo:

1. Je, kuna umuhimu wowote wa kufundisha stadi za maisha shuleni? Ndiyo/Hapana (zungusha duara kwenye jibu sahihi) kama jibu ni ndiyo, kwa nini?

Jibu: Ndiyo, kwa sababu siyo wanafunzi wote wamebarikiwa kitaaluma, kiakili kuweza kuelewa vyote vinavyofundishwa darasani. Kwa kupitia haya maarifa tutakayojifunza kwenye stadi za maisha kwenye hizi klabu itatusaidia kuwa na wigo mpana wa uchaguzi wa shughuli tutazofanya tusipofanikiwa kuendelea na masomo ili kujikimu kimaisha .

Stadi za maisha zitawasaidia wanafunzi kufanya maamuzi sahihi, kuendelea tabia nzuri, kutatua

matatizo, kuwa na ujasiri na kujiamini.

2. Klabu ina tofauti gani na mafundisho yanayotolewa darasani?

Jibu: Klabu huwa inatupatia nafasi ya kujifunza vitu ambavyo hatufundishwi darasani, tunaweza kuchangia mawazo yetu kwa uhuru na kuchangia mawazo ambayo yanagusa maisha yetu tofauti na mafundisho ya darasani.

3. Ni kitu gani ambacho klabu hutoa ambacho darasani hakipatikani?

Kujihusisha kwenye kazi za jamii moja kwa moja, stadi za maisha, ujasiri na kujiamini, uhuru wa kuchangia mawazo na uhuru wa kujieleza, inasaidia tunaweza kushiriki shughuli za kijamii, kushirikiana nk.

4. Ni mada zipi za stadi za maisha ambazo wanafunzi wangependa kujifunza?

Kujiamini, mawasiliano fanisi, ujasiriamali, kuweka na kuandaa malengo ya maisha..

5. Tunawezaje kutua klabu za shule kufundishia Stadi za maisha?

Wanafunzi walijibu vyema haya maswali yote. Hayo ni baadhi ya majibu machache yaliyotolewa na wanafunzi. Kulingana na majibu waliyotoa kuna umuhimu mkubwa wa kupata elimu ya stadi za maisha kwa wanafunzi wa sekondari. Mwaka unaokuja tutaweza kuwaunganisha na mashirika yanayotoa mafunzo mashuleni na wanaotoa misaada kwa ajili ya kuwezesha shughuli za kijamii.

Mashindano ya Insha, kutengeneza mabango yenye ujumbe unaohusu elimu, haki za watoto na hotuba. Mashindano haya yatahusisha wilaya ya Arusha mjini, Meru, na Arumeru.

Vigezo na taratibu za kushiriki zitatolewa mwezi wa nne.

Interested? Email Hilda@thefoundationfortomorrow.org or send a message through SMS to +255 752 534 102.

Habari kutoka Mashuleni

Darasa Saidizi la K.K.K

**By: Mwalimu Maganga Lorry
Shule ya Msingi Mbaaseni**

Darasa saidizi la K.K.K ni nini?

Ni darasa la wanafunzi ambao hutoka katika madarasa mbali mbali wenye uwezo duni katika kujifunza stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu.

Kuanzishwa

Darasa hili lilianzishwa mnamo mwaka 2009 mwezi Julai likifundishwa na walimu wawili ambao ni mwalimu Monyaichi I. Shayo pamoja na mwalimu wa kujitolea Nambari Lorry chini ya usimamizi wa uongozi wa uongozi wa mwalimu mkuu, Maganga D. Lorry.

Malengo

1. Darasa hili lilianzishwa kwa lengo la kuondoa tatizo la kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na orodha.
2. Mwanafunzi afikapo darasa la saba awe anauwezo wa kusoma, kuandika, kuhesabu na orodha.
3. Mwanafunzi amudu masomo ya sekondari kwani atakuwa na msingi imara kutoka shule ya msingi.

Uendeshaji wa Darasa Saidizi

Kipindi hichi cha K.K.K (Kusoma, kuandika na

Kuhesabu) huwa kinaendeshwa baada ya vipindi vya darasani, hinyo mwalimu muhusika akishirikiana na walimu wengine wanawashirikisha wanafunzi kutoka kila darasa ambao wana tatizo la K.K.K (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) na kuwapanga katika makundi ili kurahisisha kazi.

Hatua za kufundisha watoto hawa ni kama zifuatazo:

Watoto hawa hufundishwa kwa namna mbalimbali kwa mfano,

- a) Kuwafundisha kwa vitendo kwa kutumia michoro hewani kisha wanafunzi kuiga vitendo hivyo kwa mfano kuandika herufi 'a'.
- b) Kuwafundisha kwa vitendo kwa kutumia michoro ardhini mfano kuandika namba '2'.
- c) Kuwafundisha kwa vitendo kwa kutumia vibao
- d) Mwishowe kuandika wenyewe katika daftari

Baada ya hapo walimu huwatembelea wanafunzi kwa vikundi kuhakikisha kila mmoja anaelewa na mwenye matatizo anasaidiwa. Hapo hapo mwalimu husika hutoa tathmini kuona wale ambao hawakuweza na walioweza, wale ambao hawakuweza husaidiwa tena kwa mfano huohuo na kwa walimu hao hao kwa muda mwingine mpaka waelewe.

Umuhimu Wa Darasa Saidizi

Kuna umuhimu wa kuwa na darasa saidizi la K.K.K (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) umuhimu huo ni:

1. Humuwezesha mwanafunzi kuweza kujua kusoma, kuandika na kuhesabu ili kuweza kuendana na wenzake ambao walifahamu K.K.K
2. Mwanafunzi atamudu masomo yake darasani bila matatizo yoyote kwa sababu mwanafunzi anatakuwa anajua hatua zote tatu kusoma, kuandika na kuhesabu
3. Imepunguza idadi ya wasiojua k.k.k (Kusoma, Kuandika na kuhesabu)

Mafanikio

1. Tumepunguza kwa kiwango kikubwa idadi ya wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kutoka wanafunzi 54-21 kwa mwaka 2009 Desemba.
2. Tumefanikiwa kufaulisha wanafunzi wa darasa la VII kwa sababu wanafunzi wote wanauwezo wanauwezo wa kusemo na kuelewa vyema masomo yote

(continued)

Darasa Saidizi la K.K.K.

Changamoto

Pia katika darasa hili la k.k.k kuna changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

1. Kazi hii inahitaji nguvu ya ziada hivyo shule inatakiwa kuwa na walimu wa kutosha.
2. Mwalimu na mwanafunzi huchoka kutokana na vipindi vya asubuhi mpaka alasiri
3. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia mfano. Vitabu vya k.k.k chati mani
4. Wanafunzi wenye umri mkubwa kujiona wanadhaliika kuchanganywa pamoja na wenye umri mdogo
5. Wanafunzi wa k.k.k kupotezewa muda wakati wakiwa kwenye madarasa ya kawaida kwa kuwa hawaelewi walimu

Learning Support Unit Project: Helping Children Cope in School By: Madam Eva Ngowi, Headmistress, Usa River Academy Primary Section

After the SOPAA (System-Oriented Plan for Academic Achievement) Model training that was held by The Foundation for Tomorrow on 21st and 22nd May 2015 we went ahead and started a Learning Support Unit (LSU) in our school.

In this unit we offer advice and support to parents, pupils, and teachers in the areas of emotional, social, and behavior learning difficulties.

The unit exists to keep this affected pupil in school and working while seeking to address their wide range of problems as referred by the class teachers. The key purpose of LSU is to foster the development of independent and life long learn

What kind of child needs the services of the learning support unit?

An LSU placement will be considered for children whose behaviour is a barrier to them being able to successfully access the routines and curriculum of a mainstream classroom.

These types of behaviours may include:

- Children whose known early or recent history suggest that they may be at risk
- Children who are very restless, cannot listen, hyper vigilant, behave impulsively or aggressively.
- Children who are withdrawn and unresponsive and having difficulty relating to others.

Tips on how to make LSU effective a successful one:

- Build a good relationship with pupils to foster essential successful motivation
- Break down learning tasks into small steps which lead to success.
- Ensure that the learning support unit has interesting displays which are used as part of the learning process
- Share, reinforce and review the objectives of learning with the learners themselves.
- Evaluate what they have done so far and improvements to be made.

I thank TFFT for the training, for it has been tremendous since the improvement of struggling learners was highly noted since we implemented this project.

TFFT

**Ikisherekea
Siku ya Mtoto ya
Umoja wa
Mataifa: Makao
12 ya watoto
yalipongezwa**

By: Hedwiga Mchaki, TFFT
Psychosocial and Health
Program Manager



Katika kuadhimisha Siku ya Watoto ya Umoja wa Mataifa inayoadhimishwa tarehe 20, ya mwezi Novemba kila mwaka, Kwa mwaka huu 2015 Shirika la The Foundation For Tomorrow limevitunuku tuzo vituo bora vya makao ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi katika mkoa wa Arusha. Tuzo hizo zenye lengo la kutambua juhudi na mchango wa makao ya watoto katika kujenga jamii bora, kulinda na kuhakikisha usalama kwa watoto zilikabidhiwa kwa washiriki na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa wa Arusha Bi. Blandina Nkini kwa niaba ya mkuu wa mkoa wa Arusha.

Zoezi hili lilianza mwezi Novemba 2015 kumtafuta atakaekidhi vigezo na kuchukua tuzo hiyo ya makao ya watoto. Mchakato ulianza kwa kutumia vyombo vya habari. Tilitumia Radio Sunrise kutangaza kueleza nini hasa tumepanga kufanya na vipi wenye makao ya watoto wanaweza kushiriki katika kuwania tuzo hiyo.

Mwishoni mwa mwezi Oktoba tulipokea maombi ya vituo vitakavyoingia kwenye kinyang'anyiro hicho. Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Novemba tulikamilisha kupokea maombia hayo. Tulianza kupitia vituo tukisaidiana na Maafisa wa ustawi wa jamii wa wilaya husika kujidhibitishia viwango vye vituo tulivyopokea tukivilinganisha na vigezo vilivyowekwa na serikali na vinavyotumika na maafisa ustawi kukagua na kusajili vituo vya makazi ya watoto. Tulipokea maombi kutoka katika wilaya 3, hizi ni Karatu, Monduli na Meru.

Vituo vya makao ya watoto vipatavyo 12 kutoka wilaya za Meru, Monduli na Karatu vilishiriki katika mchakato wa tuzo hizo kwa mwaka huu, ambapo kituo cha SMALL STEPS FOR COMPASSION (www.smallstepsforcompassion.org) kilichopo Usa River wilaya ya Meru ndicho kilichoibuka mshindi wa jumla kimkoa, huku kituo cha RIFT VALLEY CHILDREN FUND (www.tanzanianchildrensfund.org) kilishinda tuzo ya mshindi wa

wilaya ya Karatu na MAJENGO CHILDREN'S HOME (www.majengo.org) chenye makao yake katika mji wa Mto wa Mbu kikiwa mshindi wa wilaya ya Monduli.

Vituo vingine vilivyoshiriki ni Falco's Children-Village, Havilah Children Home, STEMM, SEEWAY TZ, Huruma Children's Home, Happy Watoto Kikatiti, Rhotia Valley Children Fund, Shaloam Children Center and Children Concern Foundation.

Akizungumza katika hafla ya utoaji wa tuzo hizo, iliyofanyika katika ofisi ya shirika hilo jijini Arusha, Bi. Nkini alisema kuwa uangalizi wa watoto ni muhimu sana katika ustawi wa taifa kwa kuwa ndio unaojenga msingi wa taifa kwa kuwapa watoto malezi bora. "Viongozi wa taifa letu hutokana na malezi na makazi bora waliyoyapata utotoni", alisema.

Naye mkurugenzi mkazi wa shirika la TFFT ndugu, Kennedy Oulu aliwahimiza washiriki wa



tuzo hizo kuendelea kuunganisha juhudi zao katika kushughulikia changamoto ziwapatazo watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

"Inahitaji huruma, upendo na msukumo wa kweli katika kuwasaidia watoto hawa. Licha ya kuwa tatizo la watoto waishio katika mazingira magumu na hatarishi ni kubwa na ni vigumu kutokomeza, muunganiko wa juhudi za kila mmoja wetu litawezesha kuweka mchango mkubwa katika kupunguza tatizo lililopo", alisema Oulu.

Aidha Oulu aliongeza kuwa, haki za watoto katika nchi yetu zinakiukwa sana, si kwa watoto waishio katika mazingira hatarishi tu, bali hata kwa wale wasio katika mazingira hayo. Aliongeza kuwa, tafiti zinaonesha kwamba kuna ukiukwaji mkubwa zaidi kwa watoto waishio kwenye makao ya watoto kuliko walio majumbani na sehemu zingine. Hili linatokana na dhamira na malengo tofauti ya wale wanaoanzisha na kuendesha makao hayo.

"Haki za watoto zinakiukwa kwa sababu wanajamii kwa kiasi kikubwa hawatambui kuwa watoto pia wana haki zao! Sheria za watoto (LCA 2009) zimeweka wazi haki za mtoto na matokeo ya ukiukwaji wake. Sisi tunaowalea watoto na jamii kwa ujumla hatuna budi kuzitambua, kuzifuata na kuhakikisha utekelezaji wa haki za watoto". Alisema Oulu.

We want to hear from you! If your school has newsworthy events, projects you are proud of, or thoughts you want to share that would benefit your fellow educators and other school managers, send them to us and we will publish them in the next edition of Tufundishane! Articles that talk about best practices will be given preference, but we also welcome literary contributions such as essays and poems from educators and students.



Physical Address:
2nd Floor, King Solomon House
Anglican Church Compound

For comments/suggestions, email:
Noah@thefoundationfortomorrow.org

Or message/call: +255 753 661 770



This year The Foundation for Tomorrow (TFFT) is celebrating its tenth year. For a decade, TFFT's work can be encapsulated in one word—"THRIVE." Our work is about empowering Most Vulnerable Children (MVC) to thrive and reach their fullest potential and contribute to improving their communities.

Through our Scholarship Program, Psychosocial and Health Program, Teacher Training Program, and Full Circle Program, most vulnerable children thrive into the actualization of this reality in their lives.

We would love for the local community in Tanzania to participate in this pursuit. Together we can address the challenges these children face and ensure their access to quality education and medical care, safeguard their wellbeing ensuring they are free from harm and abuse, and equip them with all the necessary life skills they need to thrive. There are so many ways you can help.

SCHOLARSHIP PROGRAM

Provide most vulnerable children access to quality education



PSYCHOSOCIAL AND HEALTH PROGRAM

Provide access to healthcare and improve MVC households through the Household Economic Strengthening Project (Wezesh Kaya)

TEACHER TRAINING PROGRAM

Equip teachers with necessary skills to deliver quality instruction

FULL CIRCLE PROGRAM

Equip children with necessary life skills for them to thrive in life.

YOU CAN BE A PART OF THE TFFT STORY.

We welcome donations in cash or kind to help us expand the reach of our programs. And if you feel you can make a positive impact on a youth's life through life coaching or mentoring, we would love to hear from you!

Contact: Anton@thefoundationfortomorrow.org | Mob: +255 763 970495